

Anuani ya simu: “UCHUNGUZI”,

Simu Nambari: (026) 2782777,
Nukushi: (026) 2782777,
Barua pepe: rbcnjombe@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz



Mkuu wa TAKUKURU (M),
Mkoa wa Njombe,
Mtaa wa Kwivaa,
S. L. P 629,
59101 NJOMBE.

NJOMBE - APRILI 17, 2020

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MAHAKAMANI KWA WIZI WA KUTUMIA MASHINE ZA POS SHS 99,321,466/-

Katika suala la kudhibiti vitendo vya rushwa ofisi ya TAKUKURU Njombe imebaini kuwa bado tunalo tatizo kubwa kwenye eneo la ukusanyanyaji wa maduhuli ya Serikali hasa kwa wakusanya mapato waliowekwa na Halmashauri zetu katika maeneo mbalimbali kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato za POS. Wajanja wachache wanaijumu Serikali na mapato kuishia mifukoni mwao. TAKUKURU Njombe tumefanya uchunguzi na hadi sasa tumeweza kuwafikisha watuhumiwa saba mahakamani.

Mnamo tarehe 15/4/2020 TAKUKURU imewafikisha katika mahakama ya Wilaya ya Makete Maafisa saba - Watendaji wa vijiji kwa wizi wa fedha za Halmashauri ya Wilaya ya Makete ambazo zilikuwa ni makusanyo ya mapato ya Halmashauri kwa kutumia mashine za POS (POINT OF SALE- ELECTRONIC MACHINES).

Kesi zilizofunguliwa mahakamani za Maafisa Watendaji hao wa vijiji ni;

1. **CC.12/2020** Jamhuri dhidi ya **Chrispin Raphael Ngonela** Mtendaji wa kijiji cha Matamba Wilayani Makete anayeshatikiwa kwa kosa la wizi wa jumla ya shs. **24,356,656/=**.
2. **CC.13/2020** Jamhuri dhidi ya **Exavery Pius Mwabena** Mtendaji wa kijiji cha Ikungula Wilayani Makete anayeshatikiwa kwa kosa la wizi wa jumla ya shs **3,038,022/=**.
3. **CC.14/2020** Jamhuri dhidi ya **Elia Mose Nguvula** Mtendaji wa kijiji cha Ndapo Wilayani Makete anayetuhumiwa kwa kosa la wizi wa jumla ya shs **7,968,060/=**.
4. **CC.15/2020** Jamhuri dhidi ya **Benson Anyingisye Mbwilo** Mtendaji wa kijiji cha Ludodolelo Wilayani Makete anayetuhumiwa kwa kosa la wizi wa jumla ya shs **16,220,098/=**.
5. **CC.16/2020** Jamhuri dhidi ya **Salim Saleh Salim** Mtendaji wa kijiji cha Kisinga Wilayani Makete anayetuhumiwa kwa kosa la wizi wa jumla ya shs **28,212,970/=**.

6. **CC.17/2020** Jamhuri dhidi ya **Ebson Issa Mahenge** Mtendaji wa kijiji cha Mbalache Wilayani Makete anayetuhumiwa kwa kosa la wizi wa jumla ya shs **14,350,160/=**.
7. **CC.18/2020** Jamhuri dhidi ya **Victor Frank Mapunda** Mtendaji wa kijiji cha Iindiwe Wilayani Makete anayetuhumiwa kwa kosa la wizi wa jumla ya shs **5,175,500/=**.

Hivyo jumla ya kiasi cha fedha kilichoibwa na Watumishi hawa kupitia mashine za POS ni jumla ya **Shilingi 99,321,466/-**

Watuhumiwa wanne ambao mashtaka yao yanazidi shilingi milioni kumi (10) wamekosa dhamana kwa kushindwa kutimiza masharti ya dhamana yaliyowekwa na mahakama hiyo ikiwa ni pamoja na kuweka nusu ya fedha ambazo zinatuhumiwa kuibwa na watuhumiwa hao ikiwa ni matakwa ya kisheria chini ya Kifungu cha 148(5)(e) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 marejeo ya mwaka 2002.

Natoa wito kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata na watu wote walioaminiwa na Serikali kukusanya mapato ya Halmashauri katika mkoa wa Njombe wawe waadilifu katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kuwasilisha kwa usahihi fedha zote katika akaunti za Halmashauri kwani TAKUKURU Mkoa wa Njombe bado inaendelea na uchunguzi dhidi ya vitendo vya rushwa na wizi katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa mfumo wa POS (POINT OF SALE-ELECTRONIC MACHINES) na wote watakao bainika kufanya ufujaji na wizi wa fedha za mapato watachukuliwa hatua kali ikiwemo kuwafikisha mahakamani.

Hivyo TAKUKURU Mkoa wa Njombe inawataka wananchi na watumishi wote wa umma kuwa wazalendo na kuungana na Serikali katika vita dhidi ya Rushwa ili kujenga na kukuza uchumi wa Mkoa wetu na Taifa kwa ujumla.

Taarifa imetolewa na;

Bi. Domina Mukama,

**Mkuu wa TAKUKURU (M)
Njombe**